**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA TATU

***(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)***

**20 NOVEMBA, 2014**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI SABA**

**KIKAO CHA KUMI NA TATU – 20 NOVEMBA, 2014**

## I. DUA

Naibu Spika, Mhe. Job Y. Ndugai alisoma Dua saa 3.00 Asubuhi na kuliongoza Bunge.

MAKATIBU MEZANI

1. Ndg. John N. Joel

2. Ndg. Neema Msangi

3. Ngd. Hellen mbeba

## II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU

Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri Mkuu Maswali ya papo kwa papo:-

1. Mhe. David Ernest Silinde
2. Mhe. Moses Machali
3. Mhe. Eng. Mohammed Habib Mnyoa
4. Mhe. Dkt. Goodluck Ole Medeye
5. Mhe. Dkt. Anthony G. Mbassa
6. Mhe. Iddi Mohamad Azzan
7. Mhe. Masoud Abdallaha Salim

## III. MASWALI YA KAWAIDA

### 1. OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali namba 152. – Mhe. Nyambari C.M. Nyagwine

Nyongeza i. Mhe. Nyambari C.M. Nyangwine

Swali 153 – Mhe. Dkt. Antony G. Mbassa

Nyongeza – i. Dkt Antony G. Mbass

**2. MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)**

Swali namba 154 – Mhe. Mariam Nassoro Kisangi

Nyongeza

i. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi

**3. WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**

Swali namba 155 – Mhe. Azza Hillary [kny: Masoud Suleiman Nchambi]

Nyongeza- i. Mhe. Azza Hillaly Hamad

**4. WIZARA YA FEDHA**

Swali namba 156 – Mhe. Murtaza Ally Mangungu

Nyongeza: (i) Mhe. Murtaza Ally Mangungu

Swali namba 157 – Mhe. Catherine Magige

NYONGEZA. Mhe. Catherine Valentine Magjige

Swali namba 158 – Mhe. Rajab Mohammed Mbarouk [kny. Leticia Nyerere]

NYONGEZA. i. Mhe. Rajab Mohammed Mbarook

**5. WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Swali namba 159 – Mhe. James Francis Mbatia [kny. Joshwa Samuel Nassari]

NYONGEZA i. James Francis Mbatia

Swali namba 160 – Mhe. Amina Mohammed Mwidau

Nyongeza i. Amina Mohammed Mwidau

## IV. MATANGAZO

a) Wageni mbalimbali walitambulishwa Bungeni;
b) Vikao vya Kamati za Bunge vilitangazwa kufanyika saa 7. Mchana;
c) Wabunge wote wanaalikwa katika Ibada ya kumtawaza Askofu wa 6 wa Diosis wa Kanisa la Anglikana tarehe 23/11/14 saa 3 Asubuhi.

## V. MIONGOZO YA SPIKA

1. Mhe. Clara Diana Mwatuka aliomba mwongozo na kuuliza kwanini Serikali inawatumia Walimu kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao wanalazimika kuacha kufundisha, ilihali kuna vijana wanaishi ambao hawana ajira hivi sasa?

   KITI: Jambo hili halijakaa Kimuongozo ila serikali imesikia itaaweza kutoe maelezo;

2. Mhe. Martha Moses Mlata aliomba mwongozo kuwa kufuatia ubinafsishaji wa iliyokuwa kartini ya Bunge, ni kwa nini vijana waliokuwa wanafanya kazi katika kantini hiyo wameachwa wakitangatanga bila ajira yoyote.

   KITI: Suala hili liko mikono salama ya Tume ya Bunge na baadhi ya Vijana hao wameshapatiwa kazi zingine na wengine wanaenda leo kushughulikiwa;

3. Mhe. David Zacharia Kafulila aliuliza kuwa kuna fununu kwamba kuna mkakati mkubwa unafanywa wa kuitumia Mahakama kuzuia Taarifa ya CAG kupitia Kamati ya PAC isijadiliwe.

   KITI: ufafanuzi wa jambo hili utatolewa hapo baadaye.

4. Mhe. Juhaga Joelson Mpina aliuliza kwanini Muswada wa VAT hauletwi Bungezni licha ya kuwekwa kwenye ratiba ya Bunge.

AG: Muswada utashughulikiwa katika Bunge hili na Ikawezekana hata kesho unaweza kuletwa Bungeni;

5. Marganeth Simwanza Sitta aliomba mwongozo kwamba kufuata Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali uliopangwa kujadiliwa leo Bungeni kuwa na mapendekezo ya kurekebisha vifungu vya sheria ya Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya juu, Kamati ya Huduma ya Jamii haikubaliani kabisa na mapendekezo hayo hivyo alitaka kujua kama vifungu vya sheria hiyo vitajadiliwa.

KITI: Hakikuwa na taarifa juu ya jambo hilo, hivyo shughuli hiyo ya Muswada inaahirishwa mpaka saa 11.00 jioni, ili kutoa muda kwa Kamati ya Huduma za jamii; Katiba, Sheria na Utawala, AG, pamoja na Mbunge yeyote atakayehitaji wakutane na wajadiliane na kukubaliana juu ya jambo hilo.

6. Mhe. Rukia Kassim Ahmed aliomba mwongozo Kufuatia uamuzi wa Hazina kulipa moja kwa moja mishahara ya wafanyakazi wa Serikali ikiwemo Wabunge, kumekuwa na changamoto / kasoro zinazosababisha Wabunge kudaiwa na Mabenki kwani walikopa kupitia udhamini wa Bunge. Je, kwa kufanya hivi Selikari inajigeuza na kuhisimamia Bunge.

KITI: Tume ya Bunge itaongea na Hazina juu ya jambo hili na kuona namna bora ya kulishughulikia.

7. Mhe. Khatib Said Haji aliomba mwongozo kuuliza nini kinachoendelea kwa wawakiliishi wa Tanzania kwenye Bunge la Afrika Mashariki Kufuatia taarifa zinazosikika kuwa Mhe. Shyrose Bhanji anafanya vitendo vya ukosefu wa maadili.

- WAZIRI Jumuia ya Afrika Mashariki

  Mgogoro wa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki ndio chanzo cha migogoro/ mambo mengi yanayoendelea ambapo wabunge wa Bunge hilo wamegawanyika katika makundi mawili yaani wanaotaka aondolewa na wengine wanatetea asiondolewe. Kundi la wanaotaka Spika aondolewe wanaona Tanzania ndio kikwazo kwani awali Tanzania haikuwa na msimamo huo.

- Kilichotokea juzi kwa wawakilishi wa Tanzania, Mhe. Shyrose na Mhe. Ndarakindo kinaelezwa kwa kupotoshwa kuwa Shyrose alimpiga kibao mwenzie ukweli ni kwamba akiwa anatembea alimgonga Nderakindo ndipo kwa kusaidiana na Wabunge wa Uganda walienda kumshtaki polisi hata hivyo walipatanishwa na kuelewana.

- Kuhusu shutuma za mambo ya nyuma ya Mhe. Shyrose Bhanji, Tume ya Bunge la Afrika Mashariki inashughulikia ikimaliza Waziri atatoa taarifa kwa Spika na Bunge litaamua nini cha kufanya.

8. Mhe. Susan Jarome Lyimo aliuliza kwamba jana Waziri wa Utumishi wakati anajibu swali no. 142 alisema hakuna tatizo la Walimu wa masomo ya Arts nchini je, ni katika level gani na anawaeleza nini vijana wanaosomea masomo hayo.

WAZIRI UTUMISHI

Jibu hilo ni sahihi, tatizo hili tupo ni ugawaji wa walimu hao hivyo kuanzia sasa Serikali imejipanga kutatua jambo hilo.

KITI: Suala la ESCROW na Bunge kuingiliwa na Mihimili mingine limejitokeza sana kwa wabunge kila siku katika mkutano huu. Naibu Spika alitoa nafasi kwa

Wabunge wafuatao ili waongee kwa dk 5 kila mmoja na kushauri Kiti kwa pamoja na kamati ya Uongozi namna bora ya kulishughulikia jambo hilo.

1. Mhe. David Zacharia Kafulila
2. Mhe. Ester Amos Bulaya
3. Mhe. Michael Lekule Laizer
4. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa
5. Mhe. James Daudi Lembeli
6. Mhe. James Francis Mbatia
7. Mhe. Tundu Anthiphas Lissu
8. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe

Wajumbe waliochaangia walieleza kuwa hakuna Kanuni/Sheria wala kifungu cha Katiba kinachompa mamlaka mtu yoyote/Mhimili mwingine kuingilia madaraka ya Bunge. Hivyo kushauri kiti kulinda kinga na mamlaka ya Bunge kwa kelekeza Taarifa ya PAC kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipewa nafasi ya kutoa ushauri juu ya jambo hili ambapo alishauri kuwa Kiti na Kamati ya Uongozi vitumie busara katika jambo hili ili kuhakikisha kuwa kila Mhimili unatekeleza kazi yake.

Baada ya Ushauri huo Naibu Spika alitoa maelezo kuwa amepokea Ushauri uliotolewa na Wabunge wote na utafanyiwa kazi kwa kuhakikisha kuwa haki inatendeka.

## VI. MATANGAZO

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati ya Huduma za Jamii, pamoja na AG wakutane katika Ukumbi wa Msekwa ili kujadiliana juu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali. Vilevile aliwataka wajumbe wanaohitaji kujumuika katika Kikao hicho pia wafanye hivyo.

## VII. KUSITISHA BUNGE

Naibu Spika alisitisha Bunge saa 6.25 mchana mpaka saa 11.00 jioni

## VIII. BUNGE KURUDIA

Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia na kuongozwa na Mhe. Mussa Azzan Zungu.

## IX. HOJA ZA SERIKALI

Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2014.

- Kufuatia kutokamilika kwa mjadala wa Muswada huu, Mwenyekiti aliahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Ijumaa saa 3.00 Asubuhi na kuagiza Kamati husika pamoja na Serikali kuendelea kukamilisha kazi hiyo ili Muswada huo uingie Bungeni kesho jioni.

**DODOMA**
**20 NOVEMBA, 2014**

**DKT. T.D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**